Mwandishi: Hope Azeda
Mhariri: Saumu Mwasimba

## Utangulizi

Hujambo na karibu tena katika kipindi cha sikiliza ujifunze juu ya afya. Leo ikiwa tunaingia sehemu ya kumi na ya mwisho ya mchezo wa kuigiza kuhusu afya ambapo leo tunaangalia juu ya dawa za kulevya na madhara yake ya kiafya kwa binadamu kwa jumla. Vijana wawili kati ya marafiki watano wanakamatwa na polisi baada ya kukutikana na wakinunua dawa za kulevya. Je nini kitawatokea katika kituo cha polisi? Je wazazi wao watazipokeaje habari hizo? Je watafanikiwa kurudi kwenye bweni? Tega sikio…

## Tukio la kwanza

*Hassan na Manuel katika bweni chumbani, asubuhi. Kuna sauti za mbali, mara moja moja sauti za pikipiki au kengele za baiskeli. Radio.*

Manuel: Hassan nina wasiwasi sana kuhusu Steve na Simo. Wanaweza kuwa wako wapi?

Hassan: Usishughulike Manuel, wale ni watu wakubwa sio watoto wa kufuatiliwa.

Manuel: Lazima tufanye kitu, kama kuna tatizo lolote tutakuwa wa kwanza kuwa washukiwa wa kwanza kuhojiwa.

Hassan: Una wazimu wewe? Steve na Simo wako katika daraja nyingine bwana… huwezi kufanya chochote kuwabadilisha tabia… hawawasikizi hata wazazi wao.

Manuel: Hassan! Steve na Simo ni wenzetu, tunaishi nao hapa, wanahitaji msaada wetu. Huoni kama maisha yao yametawaliwa na ulevi wa madawa ya kulevya na hawajali

chochote sio vitabu sio chakula sio familia wala afya zao… wanaugua wanatuhitaji kwa kweli.

Hassan: Manuel nilifikiri ulisema kwamba kuwa rafiki na washikaji hawa wawili ni kupoteza muda, sasa umebadilika… Acha hizo bwana mimi usinipotezee muda hapa, nina kazi nyingi za kufanya.

Manuel: Hassan?

Hassan: Nini?

Manuel: Lazima tufanye kitu…

Hassan: Kitu kama nini?

Manuel: Unajua tunaweza kwenda tukakivuruga kile kikundi chote cha vijana wanaoamini kwamba unaweza tu kuwa maarufu ukivuta bangi na kunywa pombe kupindukia.

Hassan: Wewe unalifahamu vizuri lile kundi la vijana… wanafika mbali kutafuta madawa ya kulevya, wanatumia kila njia iwezekanayo. Halafu unaniambia mimi… mimi Hassan… niingilie dili zao? Labda nife! Tena nyamaza mimi nataka kusikiliza redio sasa! Manchester na Arsenal wapambana katika finali… (SFX Afungua redio, taarifa ya habari inasikika.)

Radio: Watu wawili wanaosemekana kuwa ni mafundi mechanika katika gereji moja huko mjini wamekamatwa wakiuza dawa za kulevya kwa kundi moja la wanafunzi sita wa shule mbali mbali. Wanafunzi hao wamekamatwa pamoja na mafundi hao wawili na wanazuiliwa katika kituo kikuu cha polisi.

Hassan: Manuel sikia… unasikia hiyo taarifa ya habari…

Radio: Majina ya mafundi hao mechanika hayajatambulika kwa sababu hawakuwa na vitambulisho vyao na wamekataa kutaja majina yao. Hata hivyo vijana waliokamatwa wanafahamika kwa majina ya Patrick, Simo kutoka shule ya

sekondari ya Green Valley. Na wengine ni Mupenzi, Matata, Steve na Frank ambao wanasemekana wanasomea shule ya upili ya St. Mathew. Wazazi, walezi na walimu wakuu wa wanafunzi hao wameombwa kuripoti katika kituo hicho cha polisi punde watakaposikia tangazo hilo. (Anazima redio)

Manuel: Hassan hayo ndiyo niliyokuwa nikiyasema. Sasa polisi inawezekana wakaja kutuhoji.

Hassan: Salaaalaa! Jamaa sasa wako pabaya… watafanya nini sijui? (Anafungua redio.)

Hassan: Polisi? Kwani ni uhalifu kusikiliza mechi? Manuel usiwe muoga kama fisi… Sisi tuko ngangari hatujalewa na isitoshe sisi hatuna hatia yoyote, kwa hivyo polisi wakija tutakabiliana nao.

**Tukio la pili**

*Polisi, mama Simo, mwalimu mkuu na Simo katika kituo cha polisi asubuhi. Kuna umati mdogo wa watu. Sauti za Walkie-Talkies zinasikika mara moja moja, kuna minong’ono kutoka kwa watu waliokusanyika, kuna shughuli nyingi kiasi.*

Polisi: (Akizungumzia umati) lazima tuseme kwamba haya yamekuwa mafanikio makubwa kwa polisi.matumizi ya dawa za kulevya kwa vijana wadogo sio tu ni jambo linalochangia gharama kubwa katika familia nyingi lakini pia kwa jamii nzima.Watoto wenu tutawaweka chini ya uangalizi kwa muda wa miezi sita.watahitajika kuripoti kila jumamosi kituo cha polisi.Tafadhalini kila mmoja apite aje hapa mbele atie saini fomu hii ya kuachiliwa kwa mtoto wake.

Mama Simo: Tadhali bwana,kuna chaguo jingine?maana sisi hatuishi hapa mjini.

Polisi: Huu ndio muda wa chini kabisa unaowezekana, madam, hakuna njia nyingine, ikiwa mwanao angekuwa zaidi ya miaka 18 tungemshtaki na kuhukumiwa, kwa hivyo hakuna kulalamika hapa... tafadhali weka saini hapa haraka niko na kazi nyingine ya kufanya mama.

SFX: (sauti za viatu mtu akitembea,na mtu anatia saini karatasi zinasikika)

Asante mama, tuonane jumamosi.

Mwalimu mkuu: Simo unaweza kunitazama machoni? Mimi ni nani?

Simo: Ni mwalimu mkuu.

Mwalimu mkuu: Na huyu ni nani?

Simo: Ni matheee

Mwalimu mkuu: Lete mikono yako (anainusa) umekuwa ukivuta bhangi kiasi gani?

(Simo anaanza kulia)

Simo: Nisamehe mwalimu, tafadhali naomba msamaha.

Mwalimu Mkuu: Simo unapaswa kuwa umefukuzwa shule muda mrefu sana unajua hilo.

Simo: Sitarudia tena mwalimu tafadhali nisamehe usinifukuze shule.

Mwalimu mkuu: Nimekasirika sana Simo kuliko wewe,unajua ni kiasi gani ninavyokupenda,siku zote umekuwa ukiipatia sifa shule yetu… umekuwa mwanafunzi mzuri katika masomo na hata katika michezo lakini sasa umeharibu kila kitu na kulitia matope jina la shule yetu, ni aibu kubwa sana!

Simo: Mama… mwalimu nisameheni! Sitarudia tena… kabisa

naahidi.

Mwalimu: Haiwezekani Simo! Nimekulinda vya kutosha. Uliniahidi utabadilisha tabia lakini hukufanya hivyo. Na kwa hivyo hakuna njia nyingine isipokuwa kukufukuza shule. Samahani sana. Na nakutakia kila la kheri katika maombi yako ya shule nyingine!

SFX: Anasukuma kiti… anaondoka

Mama Simo: Sasa mwanangu unataka nimwambie ni babako? Nitaanzaje mwanangu… enhe, maisha yako ya baadae yatakuwaje Simo?

Simo: Mama….

Mama: Usiniiite mama sasa hivi! Funga domo lako hilo… mtazame macho yake yalivyo mekundu kama bundi… ni kama hujalala wala kula kwa siku kumi….

Simo: Mama tafadhali? Polepole! Usizungumze kwa sauti kubwa rafiki zangu watasikia ukinipigia kelele.

Mama: Wacha wasikie! Sijali mimi. Ni nini hatujakufanyia Simo? Tumekunyima nini mwanangu… niliuza mbuzi wangu wote ili nipate kukusomesha, nikiwa na matumaini kwamba siku moja mwanangu na wewe utatukomboa kutoka kwenye huu ufukara tulonao... tazama sasa mwanangu… (analia) Hivi… hivi… Simon ndo malipo yako haya…?

**Tukio la tatu**

*Hassan, Simo, Manuel na mama Simo katika bweni la Mandela, saa 11.00 asubuhi. Kwa mbali sauti za watu zinasikika, mara moja moja unasikia sauti za pikipiki na kengele za baiskeli.*

Mwandishi: Hope Azeda
Mhariri: Saumu Mwasimba

Hassan: Oh Simo, ni wewe! Karibu mshikaji Mandela Ghetto... tuna…

Simo: Mambo vipi Hassan, sema Manuel! Ni mimi kwani mwadhani ni nani tena! Nilikuwa nyumbani.

Manuel: Ulikuwa nyumbani? Kituo cha polisi ndo kwenu siku hizi?

Hassan: Acha hizo Simo, usitudanganye mzee! Tumeipata kanda yote, tena redioni. Huyu ni mamako? Habari mama!

Mama: Hamjambo vijana! Simo fanya haraka kufunga mizigo yako twende. Lazima tuwahi basi la mwisho.

Simo: Nimemaliza mama.

Mama: Mizigo ni hiyo tu? Viko wapi vitu vyote tulivyokupa? Ulivipiga bei sio? Twende nyumbani kwanza. Tutazungumzia huko halafu utakutana na babako tena utamueleza babako maisha yako ya baadae yatakuwaje umesikia? Ikiwa utakuwa tayari kurudi shule au ukiwa unataka kuzururazurura mitaani.

Simo: Nakuahidi mama, nataka kuendelea na masomo! niamini! Washikaji kwa herini bakini salama. Tutaonana tena, wazazi wangu watakaponipatia shule nyingine ntarudi mjini. Kuleni tano basi! (Wagongesheana tano sauti ya makofi) Jamaa jiepusheni na makundi ya mateja! Dawa za kulevya hazisaidii babu… zitawatia mashakani tu! Nishajifunza kisomo mimi. Kwaherini jamaa!

Manuel na Hassan: Freshi basi Simo kwa heri!